**BODI YA USAJILI WA WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI (AQRB)**

# SHINDANO LA INSHA KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI, MWAKA 2024/25

## TAARIFA ZA USHINDANI NA NAMNA YA KUMPATA MSHINDI

### 1.0 Utangulizi:

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ni Taasisi ya Serikali inayosimamia Sheria Na.4 ya mwaka 2010. ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na mojawapo ya shughuli zake ni kusajili na kuratibu mienendo ya wataalamu katika fani za Ubunifu Majengo na, Ukadiriaji Majenzi hapa Nchini.

Ili kukuza uelewa kwa jamii hasa kwa Wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari, Bodi imeona ni vyema mwaka huu kuwashirikisha tena wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari (kidato 1 hadi 6) kuandika Insha kueleza jinsi wanavyozielewa fani za Ubunifu Majengo (Architecture) na Ukadiriaji Majenzi (Quantity Surveying) lengo likiwa ni kupanua ufahamu wa taaluma hizi na kuweza kuwashawishi ili wasomee fani hizi baada ya kumaliza masomo yao ya sekondari.

### 2.0 Sifa za Kushiriki:

Wanaoruhusiwa kushiriki mashindano ya Insha ni wanafunzi walio katika shule za Msingi na Sekondari Tanzania Bara**.**

### 3.0 Insha zinahusu nini?

**(a)Shule za Msingi;**

(i) Kwa uelewa wako elezea ni Ujenzi wa majengo ya aina gani yanahusisha Wabunfu Majengo na Wakadiriaji Majenzi hapa Tanzania?

(ii) Elezea lini na wapi ulisikia habari za wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi hapa Nchini.

**(b) Shule za Sekondari (kidato 1-4)**

(i) Taja na ueleze aina ya waendelezaji wanaoweza kutumia Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi.

(ii) Taja na elezea majukumu ya waendelezaji uliowataja kwa ufupi.

(iii) Kwa uelewa wako ni masomo yapi yanayofundishwa Sekondari na yanafanana hasa na fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi.

(c) **Shule za Sekondari (kidato 5-6)**

(i) Taja na elezea vifaa anavyoweza kutumia Mbunifu Majengo wakati anatekeleza kazi zake za kitaalam.

(ii) Taja na elezea vifaa anavyoweza kutumia Mkadiriaji Majenzi wakati anatekeleza kazi zake za kitaalam.

(iii) Taja vyuo vikuu vitatu vinavyofundisha fani za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi.

(iv) Taja fani mbili (2) zinazofanana na fani ya ubunifu majengo.

(v) Taja fani mbili (2) zinazofanana na fani ya Ukadiriaji Majenzi.

### 4.0 Lugha na Namna yakuandika

Lugha itakayotumika katika kuandika Insha ni Kiswahili/kiingereza. Mwandishi anaweza kuomba ushauri kutoka kwa mtu yeyote. Insha iandikwe kwa mkono, **Isipigwe Chapa** mahali popote. Maandishi yasizidi **kurasa tatu** katika karatasi nyeupe zenye ukubwa usiozidi sentimeta 21 kwa 30(‘A4 size’).

**Angalizo:** Wanafunzi watakaokiuka masharti watafutiwa matokeo yao.

### 5.0 Namna ya kumpata mshindi:

5.1 Vigezo vitakavyotumika katika Kuamua

Jopo la Waamuzi litachambua uelewa wa mwanafunzi kuhusu mada na mambo ya utambulisho.Pia waamuazi wataangalia uzingatiaji wa masharti yaliyoainishwa kwenye Tangazo.

.

**5.2 Mgawanyo wa Alama Zitakazotolewa Kuamua Washindi** :

Alama za maamuzi zitakuwa Kama ifuatavyo;

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mwandiko na urahisi wa kusomeka | 5 |
| 2. | Uelewa wa somo linalolengwa | 20 |
| 3. | Uhusiano wa kilichopo kwenye Insha na somo lenyewe | 40 |
| 4. | Matumizi ya Lugha | 15 |
| 5. | Mantiki katika mtirriiko wa mawazo | 20 |

### 6.0 **Zawadi**

**6.1 Shule za Msingi.**

| Washindi | Zawadi |
|---|---|
| Wa Kwanza Kitaifa | 300,000= |
| Wa Pili Kitaifa | 200,000= |
| Wa Tatu Kitaifa | 100,000= |
| Washindi wa kila Mikoa | 100,000= |
| Shule itakayotoa Mshindi wa Kitaifa | 300,000= |
| Shule itakayoongoza idadi ya Washiriki | 300,000= |

**6.2 (kidato 1 hadi 4)**

| | |
|---|---|
| Wa kwanza Kitaifa | 500,000= |
| Wa Pili Kitaifa | 300,000= |
| Wa Tatu kitaifa | 200,000= |
| Washindi wa Mikoa | 100,000= |
| Shule iitakayotoa mshindi wa kitaifa | 300,000 |
| Shule itakayoongoza katika ushiriki | 300,000= |

**6.3 Kidato (5 hadi 6)**

| | |
|---|---|
| Wa kwanza Kitaifa | 500,000= |
| Wa Pili Kitaifa | 300,000= |
| Wa Tatu KItaifa | 200,000 |
| Washindi wa Mikoa | 100,000= |
| Shule itakayotoa mshindi wa kitaifa | 300,000= |
| Shule itakayoongoza | 300,000= |

| katika ushiriki | |
|---|---|

**7.0 Utambulisho wa Mwanafunzi.**

Taarifa za mwandishi zijazwe
Katika fomu iliyoambatanishwa
Na kupigwa muhuri na mkuu wa
Shule baada ya kuhakikishiwa na
Mwanafunzi

**8.0 Mwisho wa Kupokea Insha na Utoaji wa Matokeo:**

**Tarehe 31 Augosti, 2024** ni mwisho wa kupokea Insha.

**9.0 Namna Ya Kutuma:**

Insha iwekwe kwenye bahasha ikiambatanishwa na fomu iliyofafanuliwa hapo juu (7.0). Juu ya bahasha andika anwani ifuatayo:-

**‘SHINDANO LA INSHA MWAKA 2024/25’**

Msajili,
Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi(AQRB)
Makao Makuu Dodoma
9 Mtaa wa AQRB,
41101 tambukareli,Dodoma.
Simu +255 262160370;
Barua pepe info@aqrb.go.tz
Tovuti www.aqrb.go.tz

**Insha ziwasilishwe Kwa njia ya Posta barua pepe au Kwa mkono katika ofisi za Bodi zilizopo Dodoma S.L.P 2377,Dar Es Salaam Ghorofa ya pili jengo la Tetex S.L.P 72673, Mwanza S.L.P 807 Railway RD, Mbeya S.L.P 635 au Arusha S.L.P 11604 Wachaga RD .**

Washindi watatu wa ngazi ya Kitaifa watachukua zawadi zao mahali na siku iliyopangwa na Bodi kutoa zawadi ikiwa watapenda kufanya hivyo. Bodi itagharamia usafiri na malazi kwa washindi hao..

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na Ofisi ya **Msajili** kwa anuani iliyotajwa hapo juu.Tangazo pia linapatikana kwenye Tovuti ya Bodi.(www.aqrb.go.tz)

**BODI YA USAJILI WA WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI**

***(Chini ya Sheria Na. 4 ya Mwaka 2010)***

(Fomu ya Kiambatanisho ya Insha)

| **TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI** | | |
|---|---|---|
| **JINA LA SHULE** | | |
| **ANU ANI YA SHULE** | | |
| **KATA SHULE ILIKO** | | |
| **TARAFA SHULE ILIKO** | | |
| **WILAYA NA MKOA** | **WILAYA** | **MKOA** |
| **JINA LA MWANAFUNZI**<br>(Andika majina matatu) | | |
| **UMRI WA MWANAFUNZI** | | |
| **JINSIA**<br>(Weka alama ya tiki √) | **MWANAUME** | **MWANAMKE** |
| **DARASA / KIDATO** | | |
| **JINA LA MZAZI / MLEZI** | | |
| **ANUANI NA NAMBA YA SIMU YA MZAZI / MLEZI** | | |
| **JINA LA MWALIMU MKUU** | | |
| **NAMBA YA SIMU YA MWALIMU MKUU** | | |
| **BARUA PEPE YA MWALIMU MKUU** | | |
| **SAHIHI YA MWALIMU MKUU** | **SAHIHI** | **MUHURI WA SHULE** |